

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA

MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 28/10/2021

KUHIDHINISHA FEDHA ZA UVIKO ZITUMIKE KWA FORCE ACCOUNT.

AGENDA ZA KIKAO

- 1.Kufungua kikao
- 2.Kuomba ridhaa ya matumizi ya FORCE ACCOUNT ya Tshs.**2840,000,000.00**
- 3.Mengineyo.
- 4.Kufunga kikao.

WALIO HUDHURIA

| NAMBA | JINA | CHEO |
|-------|------------------|------------|
| 01 | Shija Lyella | Mwenyekiti |
| 02 | Omary Saidi | Katibu |
| 03 | Irine Mukerebe | Mjumbe |
| 04 | Kelvin Rwegasira | Mjumbe |
| 05 | Bruno Sangwa | Mjumbe |

WASIOHUDHURIA

| NAMBA | JINA | CHEO | SABABU |
|-------|---------------|--------|------------------|
| 01 | Nestori Mjojo | Mjumbe | Safari ya kikazi |

GENDA NAMBA 1: KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao cha bodi ya zabuni saa 10:00 alasiri kwa kuwakaribisha wajumbe wa bodi na kuwataka wawe watulivu.

AGENDA NAMBA 2 :KUOMBA RIDHAA YA MATUMIZI YA FORCE ACCOUNT TSH.2840,000,000/=

Mwenyekiti alimuomba katibu asome agenda namba mbili . Katibu wa bodi ya zabuni alisoma agenda namba mbili na wajumbe walianza kujadili,Wajumbe waliomba aitwe mhandisi wa Halmashauri Pamoja na afisa elimu wa Msingi ili wathibitishe kama wanao wataalamu wa kutosha wa kuweza kusimamia mradi pia afisa elimu aeleza kama fedha hizi zimeishaingia kwenye akaunti za shule.

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA

Mhandisi wa halmashauri ndugu **Rajabu Mfinanga** alifika na kusema yeye anao wataalamu wa kutosha ambao wataweza kusimamia mradi huo na Kaimu Afisa elimu Msingi Bi. Zainabu Masoli alithibitisha ya kuwa pesa tayari zipo kwenye akauni za shule na walimu wakuu washaandika barua za kukili kupoikea fedha hizo kwa mkurugenzi wa Halmashauri.

Baada ya kutoa maelezo hayo mwenyekiti alimruhusu Mhandisi aende na wajumbe waendelee kujadili, Mwenyekiti aliwaruhusu wajumbe waendelee kujadili na ikiwezekana wakubali kwa Pamoja ili mradi uanze.

Wajumbe kwa Pamoja walikubali pesa hizo zitumike kujenga jenga madara kwenye shule za msingi na sekondari kwa kutumia force akaunti lakini wakasisitisa taratibu ,sheria na kanuni za manunuzi zifuatwe ili kupunguza hoja za ukaguzi na kuleta ufanisi.

AGENDA NAMBA 3: MENGINEYO

Mwenyekiti alimwambia Katibu asome ajenda inayofuata, Katibu alisoma ajenda namba tatu na kuwaacha wajume wachangie agenda hiyo.

Wajumbe walimueleza Katibu wa bodi afanye kazi ya kuwaelimisha wajumbe wa kamati zitakazo undwa namna ya usimamizi wa mradi, na wakasisitiza kila kamati lazima awekwe mwananchi mmoja au wawili kama muongozo wa force account uliotolewa na PPRA unayovyoelekeza .

KUFUNGA KIKAO:

Mwenyekiti wa bodi alifunga kikao mnamo saa 3:30 alasiri na kumsisitiza Katibu awe makini kwenye mradi huu kwa kutafuta wazabuni wenye sifa ili waweze kuleta bidhaa kabla ya kulipwa fedha.

Umedhibitishwa

MWENYEKITI..... Shujaa Yella
SAINI.....
TAREHE..... 23/12/2021

KATIBU..... Oumury SAINI
SAINI.....
TAREHE..... 23/12/2021